**SHIRIKISHO LA RIADHA TANZANIA (RT)**

# KANUNI ZA UENDESHAJI WA MBIO ZA BARABARANI (ROAD RACES) ZA MWAKA 2021 NA MAREKEBISHO YA MWAKA 2025

**UTANGULIZI:**

Kanuni hizi zitasomwa Pamoja na Katiba ya Shirikisho la Riadha (AT) na zitaanza kutumika rasmi kwanzia 1/1/2026. Zitasainiwa na kupitishwa na wajumbe wa Kamati ya Utendaji.

**MBIO ZA BARABARANI KATIKA KANUNI HIZI NI**

- Mbio zote za Barabarani
- Walking Race
- Mountain run
- Ultra run
- Trail run
- Cross Country.

**Mbio zote hizi zitasimamiwa na Shirikisho la Riadha Tanzania /Vyama vya Riadha vya Mikoa kwa kufuata Kanuni hizi.**

1: Mwandaaji yeyote anayekusudia kufanya mbio ya barabarani, analazimika kwanza
kufuata kanuni na sheria zote za nchi zinazohusu matukio ya kimichezo nchini, ikiwa ni
pamoja na kanuni za usajili za Baraza la Michezo la Taifa.

2: Iwapo mwandaaji anakusudia kufanya mbio kwa kutumia jina ambalo si jina lake halisi,
au jina halisi la taasisi, basi anawajibika kwanza kusajili jina hilo kama jina la biashara
kama kanuni za BRELA za usajili wa majina ya biashara zinavyoelekeza.

3: Kushika tarehe kwenye Kalenda

a) Kila mwandaaji anayekusudia kuandaa mbio kwa mwaka unaofuata anawajibika kuthibitisha tarehe ya mbio yake kwa Shirikisho la Riadha Tanzania kabla ya tarehe 1 Novemba ili kuhakikisha mbio yake inaingia kwenye kalenda ya mwaka unaofuata na atalipa Tsh 500,000/= kwa shirikisho la riadha Tanzania ya kushika tarehe.

b) Iwapo mwandaaji atashindwa kuthibitisha tarehe ya mbio yake kabla ya tarehe hiyo hapo kifungu (a) na anataka kuendesha mbio yake atalazimika kulipa Tsh 200,000/= kwa shirikisho la riadha Tanzania na Tsh 100,000/= kwa chama cha riadha mkoa

c) Iwapo mwandaaji atataka kubadili tarehe kutoka ile aliyoishika kwenye kalenda ya mwaka husika, basi atalazimika kulipa Tsh 200,000/= kwa shirikisho la riadha Tanzania na Tsh 100,000 kwa chama cha riadha mkoa ili kushika tarehe nyingine itakayokua wazi

4: Mwandaaji anaweza kusamehewa kulipa kiasi hichi cha Ada ya kuhamisha tarehe nyingine iwapo sababu ya kubadili tarehe siyo inayotokana na maandalizi ya mbio.Mambo kama kuchelewa kupokea vifaa vya mbio au kuchelewa kwa jambo lolote la maandalizi ya mbio halitamfanya mwandaaji

kutolipa ada hii,

Bali mambo kama matukio ya kiasili, mwingiliano na ratiba ya Shirikisho la riadha Tanzania

au Ratiba ya vyombo vya kiserikali inaweza kumuepusha mwandaaji na ulazima wa kulipa ada ya kuhamisha tarehe ya mbio.

5: Mbio zote zinazofanyika kwa mara ya kwanza ni lazima zilipe ada ya usajili ya Shirikisho la Riadha Tanzania ya Tsh 200,000/= na chama cha riadha mkoa Tsh 100,000/= na zitalipwa mara moja tuu.wakati kusajili wa mbio .mbio zote hata zile ambazo zilishasajiliwa, ni lazima kutimiza masharti ya Shirikisho la riadha Tanzaniai na BMT, na kulipa ada ya vyama vya riadha vya mikoa za kila mwaka kwa kiasi cha Tsh 500,000/=

## MGAWANYO WA MBIO KWA MADARAJA

6: Madaraja ya mbio za barabarani (Classification) ni kama ifuatavyo:

- International Marathon–Marathon za Kimataifa.
- National Marathon –Marathon za Kitaifa

## INTERNATIONAL MARATHON

i) Njia iwe imepimwa na kuthibitishwa na Mtaalamu anayetambulika na (WA/AIMS) na mwenye Grade A

ii) Lazima iwe na Electronic Timing System.

iii) Ada ya malipo kwa International Marathon itakuwa ni 10% ya mapato yote ya ada ya viingilio vyote vya washiriki na chama cha riadha mkoa Tsh1,000,000/=

iv) Lazima iwaalike viongozi wakuu wawili wa Shirikisho la riadha Tanzania, Rais na Katibu mkuu na msimamizi mmoja wa kamati ya ufundi. Na watagharamikiwa na mwandaaji.

v) Lazima ifuate kanuni za udhibiti wa matumizi ya madawa ya kuongeza nguvu,

vi) Mwaliko wa Wanariadha (Elites) toka nje hautakuwa na ukomo wa idadi isipokuwa tu ni washindi watatu tu wa mwanzo kwa kila nchi watastahiki kupata zawadi( only the first three Elites per country will eligible for prize money).

vii) Zawadi kwa Mshindi wa Km 42.195 isipungue Tshs 5,000,000/- na kwa 21.1 km isipungue
Tsh 3,000,000/ kwa mshindi

viii) Zawadi zitatolewa kuanzia mshindi wa kwanza hadi wa kumi na kwa mtiririko mzuri ambao utashauriwa na wataalamu wa shirikisho la riadha.

ix) Hakuna ukomo wa mwaliko kwa social Runners

x) Kabla ya kuanza kutangaza mbio, ni lazima mwandaaji awasiliane na shirikisho la riadha Tanzania ili kuhakikisha taratibu zote za awali zimefuatwa .

**NATIONAL ROAD RACES**

i. Mbio za kitaifa lazima zipimwe na mtaalamu anayetambulika na shirikisho la riadha Tanzania.
ii. Lazima kuwe na zawadi ya fedha isiyopungua Tsh 3,000,000 kwa mbio za km 42.195, na mbio za 21.1 km kuwe na zawadi isiyopungua Tsh 1,000,000 pia katika mbio za 10km kuwe na zawadi isiyopungua Tsh 500,000/=. Na zawadi zitatolewa kwa mshindi wa kwanza hadi wa kumi.
iii. Ada ya kila mwaka ya kuendesha mbio itakuwa Tsh 1,500,000/=.
iv. Hakutakuwa na mialiko kwa wachezaji kutoka nje ya nchi.(Elite Athletes)

**07. MAHITAJI YA LAZIMA WAKATI WA UENDESHAJI WA MBIO ZOTE:**

a. **Polisi**: :Ni lazima waandaaji wote kuomba kibali Polisi kwajili ya Ulinzi na usalama wa washiriki wa mbio za barabarani.
b. **Ambulance/First Aid**. Ambulance na huduma ya kwanza kwenye Mbio zote ni lazima.
c. **Ramani** ya njia za kukimbilia lazima zijulikane na kamati ya ufundi ya mkoa husika/Shirikisho la riadha Tanzania. Na iwekwe kwenye matangazo.
d. **Maji**: Huduma ya maji na viburudisho ni lazima kwenye mbio, na vituo vya maji vitakuwa kila baada ya kilometa 5 au vinaweza kuongezwa kulingana na hali ya hewa au mazingira ya tukio lenyewe

e. **Namba za Kukimbilia (BIB numbers)**: mbio zote lazima watumie namba za kukimbilia kwa washiriki wote na wavae kifuani

f. **Medali/t-shirt** : Mwandaaji atalazimika kutoa medali na t-shirt kwa washiriki wote waliojisajili

**8** Matukio yote ya mbio yatasimamiwa na waamuzi kutoka vyama vya riadha mikoa/Shirikisho la riadha Tanzania.

**9:** Mbio za kimataifa zitasimamiwa na shirikisho la riadha Tanzania na mbio za kitaifa zitasimamiwa na vyama vya riadha vya mikoa.

**10:** Gharama za waamuzi zitalipwa na mwandaaji wa mbio na idadi ya waamuzi itatokana uhitaji wa mbio husika .

**11:** Mwandaaji lazima ashirikiane na vyama vya mikoa kwa mbio za kitaifa na Shirikisho la riadha Tanzania kwa mbio za kimataifa ili kuhakikisha taratatibu na mahitaji yote ya mbio yametimizwa.

**12:** Marufuku watoto chini ya umri wa miaka 12 kukimbia mbio za watu wazima, watoto waandaliwe mashindano yao kutokana na umri wao kwa kuzingatia kanuni za shirikisho la riadha la Dunia pia watoto wa umri kuanzia 13 hadi 17 Hawatoruhusiwa kumbia mbio zinazozidi umbali wa 5km

**13:** Wandaaji wote wa mbio za kujifurahisha zinazotoza ada za ushiriki wa mbio mfano trail run ,mountain run pamoja na ultra run watalazimika kulipa ada zote

**14:** Mbio zote za kujifurahisha (fun run) zisizidi 10km.

**15.** Mwandaaji yeyote atakayeandaa mbio zozote kuanzia km10 kurudi chini na anatoza ada ya usajili/ushiriki atalipa ada ya Tsh. 1,000,000/= ya uendeshaji wa mbio kwa Shirikisho la riadha Tanzania.

a) Mwandaaji yeyote atakayeandaa mbio kuanzia km10 kurudi chini na hatozi ada ya usajili/ushiriki hatalipa ada ya uendeshaji wa mbio ila lazima mbio itasimamiwa na chama cha riadha katika mkoa husika.

b) Mbio zote za kujifurahisha (fun run)ambazo washiriki wake wanavaa namba za kukimbilia (Bib number)ni lazima waombe kibali cha mbio hata kama mwandaaji hatatoza ada ya ushiriki

**16:** Zawadi kwa washindi zilipwe kwa jinsia zote wanaume na wanawake na zitangazwe mapema siku 21 kabla ya mashindano, atakaye kiuka kanuni hii itampelekea tukio lake la mbio kuzuiwa na kukosa sifa ya kuandaa mbio hiyo kwa mwaka unaofuata

**17:** Ada ya kuendesha mbio ya kila mwaka ya shirikisho la riadha Tanzania itakuwa ni 1,500,000 kwa mbio za kitaifa za kuanzia km21.1

**18:** Mwandaaji yeyote aliyepata kibali cha kuendesha mbio kutoka shirikisho la riadha/chama cha riadha mkoa atalazimika kuweka Nembo ya shirikisho la riadha Tanzania kwenye matangazo yote ya mbio

**19:** Malipo yote ya shirikisho la riadha yatafanyika kupitia akaunti ya shirikisho la Riadha Tanzania.

**20:** Malipo ya ada ya kila mwaka ya mkoa yatafanyika kupitia akaunti za mkoa husika.

**21:** Wandaaji wote wapya lazima wawasiliane na vyama vya riadha mikoa wanakotengemea kufanya mbio zao ili wapangiwe tarehe na kupata taratibu zote za uaandaaji wa mashindano ikiwa ni pamoja na kupata kanuni za shirikisho la riadha Tanzania

22: Malipo yote ya Ada ya kila mwaka ya baraza la michezo Tanzania yatafanyika kupitia control number kutoka Baraza la Michezo Taifa (BMT) baada ya mwandaaji kukamilisha taratibu zote za awali kuanzia ngazi ya mkoa/taifa

**23:** Jina la marathon litatumika kwenye mbio za km 42.195 tu .

**24:** Jina la half marathon litatumika kwa mbio za km 21.1 tu.

**25:** Mbio chini ya km21:1 mfano 20km,10km , 5Km na 1 mile zitatambulika kama mbio za bararabani na si Marathon wala half marathon.

**26:** Matukio mawili ya mbio ndani ya mkoa mmoja kwa tarehe mmoja hayataruhusiwa.

**27:** Semina elekezi kwa waamuzi wa mbio za kitaifa lazima ifanyiwe siku mmoja kabla ya mbio kupitia kamati ya ufundi mkoa

a) Kwa mbio za kimataifa ni lazima semina ya waamuzi iwe siku mmoja kabla, kupitia kamati ya ufundi Taifa /mkufunzi wa waamuzi anayetambulika na shirikisho la riadha Tanzania/WA.

**28:** Ni lazima kila mwandaaji wa mbio za barabarani aandae mbio maalumu za watoto

(kids run) umri kuanzia miaka **12** kurudi chini na umbali kuanzia 1km ,1.5km na isizidi 2km.

a. Endapo mwandaaji kwa kushirikiana na chama cha riadha mkoa au shirikisho la riadha Tanzania wataona mazingira ya kuendesha mbio ya watoto siku ya tukio hayaruhusu itamlazimu mwandaaji kupanga siku nyingine kwa kushirikiana na chama cha riadha mkoa/shirikisho la riadha Tanzania kwa ajili ya tukio hilo la mbio.
b. Mwandaaji wa mbio atalazimika kuandaa zawadi maalumu kwa ajili ya watoto kuanzia mshindi wa kwanza hadi kumi.

c. Pamoja na mshereheshaji MC aliyeandaliwa na mwandaaji, ni lazima Mshehereshaji kutoka chama cha riadha anayeujua vizuri mchezo wa riadha kuwepo kwa gharama za mwandaaji

**Endapo mwandaaji atakiuka kanuni hizi, Shirikisho la riadha Tanzania litachukua hatua zifuatazo**

a) Onyo kali
b) kulipa Faini isiyopungua Tsh 2,000,000/=
c) Kufungiwa kuendesha mchezo wa riadha.
d) Kuchukua hatua zingine zozote ambazo shirikisho la riadha Tanzania litaona inafaa kwa kulinda heshima na hadhi ya mchezo wa Riadha.

**Kanuni hizi zitaanza kutumika kuanzia tarehe 01/01/2026**

ATHLETICS TANZANIA
17 NOV 2025
P. O. BOX 2172
DAR-ES-SALAAM

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **Rais** | **KAIMU KATIBU MKUU** |
| **Shirikisho la Riadha Tanzania** | **Shirikisho la Riadha Tanzania** |